# MAENEO YANAYOPENDEKEZWAKUANGALIWA

| Na. | Kifungu/Kipengele | Ilivyo katika Sheria ya sasa | Mapendekezo ya wadau |
|---|---|---|---|
| 1. | Jina la Sheria | • Medical Practitioners and Dentists Act. 'Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno.'<br>• Kwa kuwa Sheria inakusudia kuwajumuisha Matabibu na Matabibu Wasaidizi, ni vyema jila la Sheria likaangaliwa pia. | |
| 2. | Jina la Baraza | • Medical Council of Tanganyika 'Baraza la Madaktari Tanganyika' | |
| 3. | Muundo wa Baraza | • Ni mamlaka iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii<br>• Haina uwezo wa kumiliki rasilimali kwa jina lake. | |
| 4. | Wajumbe wa Baraza | • Mganga Mkuu wa Serikali<br>• Mwanasheria Mkuu wa Serikali<br>• Wateuliwa wa Waziri wa Afya wasiopungua 5 ambao ni madaktari. | |
| 5. | Mwenyekiti wa Baraza | Mganga Mkuu wa Serikali (Chief Medical Officer) | |
| 6. | Majukumu ya Baraza | • Licha ya kuwa na uwezo wa kusajili, Baraza halina uwezo wa kuridhia mitaala na kuzishauri mamlaka za usajili wa vyuo juu ya viwango vya elimu vinavyotakiwa.<br>• Baraza halina uwezo wa kuvikagua vituo ambavyo madaktari, madaktari wasaidizi na matabibu wanafanyia kazi<br>• Baraza halina uwezo wa kukasimu majukumu yake kwa watendaji wa ngazi za Mikoa na Wilaya (RMOs and DMOs) n.k.<br>• Baraza halina uwezo wa kuvikagua vyuo na kushauri juu ya mazingira stahiki ya utoaji elimu ya Udaktari na utabibu<br>• Baraza halina uwezo wa kuagiza au kuamua juu ya aina mavazi au alama nyingine zinazopaswa kutumiwa na daktari au tabibu | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Mtendaji Mkuu wa Baraza | • Ni mtumishi wa Umma, na huteuliwa na Mganga Mkuu Kiongozi (CMO)<br>• Sifa zake hazijaainishwa | |
| 8. | Aina za madaftari ya usajili | • Kuna aina nne za madaftari<br>- Provisional<br>- Temporary<br>- Full Registration<br>- Licenced Medical/Dental Practitioners | |
| 9. | Usajili baada ya internship | • Daktari hupewa usajili wa muda(Temporary Registration)<br>• AMO/ADO husajiliwa baada ya kuhitimu chuo, na kwamba hawana utaratibu wa internship<br>• Clinical Officers, Assistant and Clinical Officers and Dental Therapists hawatambuliwi katika Sheria ya sasa . | |
| 10. | Mitihani kabla ya usajili | • Hakuna utaratibu wa kuwatahini waombaji usajili pamoja na waliosoma na kuhitimu nje ya nchi. | |
| 11. | Leseni ya kufanya kazi za kitaaluma | • Hakuna utaratibu wa kutoa leseni za kufanya kazi za kitaaluma na pia muda wa uhai wa leseni hiyo. | |
| 12. | Elimu endelevu | • Hakuna utaratibu wa kupata elimu endelevu(Continued Professional Development- CPD), kama sharti la kupata leseni ya kufanya kazi za kitaaluma. | |
| 13. | Wigo wa kufanya kazi za kitaaluma | • Hakuna utaratibu unaomlazimisha daktari kufanya kazi ndani ya wigo wa elimu au ujuzi wake pekee. | |
| 14. | Makosa na adhabu | • Aina za makosa yanayohusiana na ukiukaji wa sheria ya madaktari au kanuni za maadali sio pana | |
| 15. | Rufaa dhidi ya maamuzi ya Baraza | • Kwa sasa rufani zote dhidi ya maamuzi ya Baraza hupelekwa Mahakama Kuu. | |
| 16. | Vyanzo vya mapato | • Vyanzo vya mapato havijatajwa | |
| 17. | Usimamizi wa Rasilimali za Baraza | • Usimamizi wa Rasilimali za Baraza haujatamkwa. | |